# STANDARD 4 MID TERM 2 EXAM 2019

# KISWAHILI

***Muda: Saa 1 dakika 40***

Ni ____1____kuyaweka mazingira yetu yakiwa ____2____. Tufyeke nyasi ____3____na kuchoma takataka. Tusipofanya hivyo, mbu na panya wataishi ____4____ nyasi hizo. Mbu ____5____ ugonjwa wa ____6____. Panya ____7____husambaza ugonjwa wa tauni ambao ____8____.

1. A. njema B. vyema C. nzuri D. zuri
2. A. masafi B. chafu C. safi D. machafu
3. A. ndefu B. refu C. mrefu D. marefu
4. A. kwa B. ndani C. katika D. katikati
5. A. huleta B. huambukiza C. huambukizwa D. hutuletea
6. A. malale B. kipindupindu C. mafua D. malaria
7. A. nao B. naye C. nayo D. nazo
8. A. ni baya B. si mzuri C. si nzuri D. ni wambaya

Kakono ____9____mtoto mtukutu. ____10____, yeye ____11____sokoni na mama ____12____. Alipokuwa njiani, alikutana na rafiki yake, Kaguu. Kaguu alikuwa amebeba chupa ____13____. Kakono alipoiona, akaitamani sana chupa ____14____. Mara tu, Kakono akampokonya Kaguu chupa yake na kukimbia nayo na kutokomea kabisa ____15____msitu uliokuwa karibu.

9. A. alikua B. hakuwa C. hakukua D. alikuwa
10. A. Siku moja B. Siku mmoja C. Wakati moja D. Usiku moja
11. A. aliendewa B. walienda C. walitumwa D. alitumwa
12. A. wake B. yake C. wao D. yangu
13. A. mzuri B. zuri C. mazuri D. nzuri
14. A. hicho B. hiyo C. hii D. hizo
15. A. katika B. ndani C. kwa D. karibu

**Jibu maswali yafuatayo kulingana na maagizo**

16. Jibu maamkizi yafuatayo.
    Habari za utokako?
    A. Nzuri B. Mzuri
    C. Zuri D. Vizuri
17. Kanusha sentensi ifuatayo
    Wewe umeandika vizuri.
    A. Wewe haujaandika vizuri.
    B. Wewe hukuandika vizuri.
    C. Wewe hujaandika vizuri.
    D. Wewe haukuandika vizuri.
18. Chagua mnyama anayeishi mahali tofauti na wengine.
    A. Fisi B. Kaa
    C. Paa D. Twiga
19. Chagua sentensi iliyo katika nafsi ya tatu.
    A. Hawataki kusoma gazeti.
    B. Sipendi kushika uchafu.
    C. Tunaomba maji ya kunywa.
    D. Unataka nini hapa?
20. Tumia kiashiria kifaacho zaidi kujazia pengo:
    Mpira wake ni
    A. hii B. ile
    C. huyo D. huo
21. Tegua kitendawili :
    Nanywa supu, nyama naitupa.
    A. Nanasi
    B. Muwa
    C. Siafu
    D. Macho

22. Ni nini wingi wa sentensi ifuatayo?
Amelifunga duka lake.
A. Wameyafunga maduka yake.
B. Wamezifunga duka zao.
C. Wamefunga duka zao
D. Wameyafunga maduka yao

23. Tumia kiulizi sahihi;
Ni mwanafunzi __________ aliyegongwa na baiskeli.
A. gani
B. upi
C. mgani
D. myupi

24. Chagua jina linalomaanisha;
Jiko la makaa.
A. Stovu
B. Seredani
C. Bilauri
D. Mbuzi

25. Jaza pengo kwa kutumia kihusishi kifaacho zaidi.
Ni vizuri kunawa mikono __________ kutoka msalani.
A. kabla ya
B. mbele ya
C. baada ya
D. wakati wa

26. Chagua kitenzi kwenye sentensi ifuatayo;
Mtoto anacheza peke yake.
A. mtoto
B. peke
C. anacheza
D. yake

27. Nomino **cherehani** Iiko katika ngeli gani?
A. KI-VI
B. A-WA
C. U-I
D. LI-YA

28. Basi la shule yetu ni
A. ndefu
B. mrefu
C. refu
D. lirefu

29. Ni maneno gani ambayo ni vitanzandimi?
A. Sima na ugali
B. Samaki na maji
C. Leo na kesho
D. Toa na doa

30. Kanusha amri hii: **Njoo!**
A. Usikuje
B. Usije
C. Nenda
D. Usiende

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 31-40***

Sherehe ya madaraka hufanywa tarehe moja mwezi wa sita kila mwaka nchini mwetu. Hii ni siku ambayo taifa letu lilipata uhuru kutoka kwenye mikono ya wakoloni. Siku hiyo muhimu hutukumbusha jinsi ambavyo wazalendo wa nchi hii walipigana kwa jino na ukucha ili kujikomboa.

Mashujaa wengi walipoteza maisha yao katika mapigano hayo. Siku hiyo inapowadia, huwa ni siku ya mapumziko kote nchini. Siku hiyo spesheli, sherehe mbalimbali huipamba nchi yetu huku kila mmoja akiwa na furaha mpwitompwito. Sherehe zenyewe hufanywa katika makao makuu ya kaunti mbalimbali au miji mikuu mbalimbali nchini.

Wanaoshiriki katika sherehe hizi huanza kujitayarisha mapema kabla ya siku yenyewe kufika. Baadhi ya wanaoshiriki huwa vikosi mbali vya askari na wanajeshi, kwaya na wanasarakasi. Kilele cha sherehe huwa hotuba ya rais ambayo husomwa na yeye au mwakilishi wake.

31. Sherehe za madaraka hufanywa katika mwezi gani?
A. Juni
B. Julai
C. Mei
D. Aprili

32. Kulingana na taarifa ni kina nani walimwaga damu?
A. Wakenya
B. Wanajeshi
C. Mashujaa
D. Wananchi



Compiled & supplied by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | **ORDER ANSWERS ONLINE** at www.schoolsnetkenya.com

33. Siku ya madaraka huwakumbusha nini wakenya?
   A. Jinsi ambavyo wazalendo walipigwa.
   B. Jinsi wakoloni walivyomwaga damu.
   C. Jinsi ambavyo wananchi wote walipigania uhuru.
   D. Jinsi ambavyo wazalendo wetu walipigania uhuru.

34. Watu waliopoteza maisha ni wale ambao
   A. wanaendelea kuyatafuta
   B. wamefariki
   C. walipigania uhuru
   D. ni wazalendo

35. Siku ya madaraka ifikapo, haya yote hufanyika isipokuwa
   A. hotuba ya rais husomwa.
   B. wanakwaya hutumbuiza.
   C. wanafunzi wote huenda shuleni.
   D. shule zote nchini hufungwa hadi muhula mpya.

36. Ni kina nani hawakutajwa kujitayarisha kwa sherehe?
   A. Maskauti
   B. Wanakwaya
   C. Wanajeshi
   D. Wanasarakasi

37. Ni nini huonyesha mwisho wa sherehe?
   A. Nyimbo za wanakwaya.
   B. Vituko vya wanasarakasi.
   C. Kwaya za wanajeshi.
   D. Hotuba ya rais.

38. Ni nani humsomea rais hotuba asipokuwapo?
   A. Wazalendo
   B. Wakoloni
   C. Mashujaa
   D. Wawakilishi

39. Mapambo ya nchi yetu siku hii muhimu hutokana na
   A. vita
   B. sherehe
   C. mapumziko
   D. hotuba

40. Taarifa hii yafaa mada gani kati ya hizi?
   A. Mapumziko nchini
   B. Sherehe ya madaraka
   C. Wanasarakasi nchini
   D. Hotuba ya rais

***Soma taarifa ifutayo kisha ujibu maswali 41 - 50***

Katika kijiji Nduni, palikuwa na mtu aliyeitwa Kitema. Mtu huyo alijulikana sana kwa wizi wa kuku wa jirani zake. Kwa sababu ya ujanja wake, hakuwahi kushikwa akiwaiba kuku hao. Usiku mmoja, jogoo wa pekee katika kijiji hicho hakuwika. Mwenye jogoo huyo alipowafungulia kuku wake asubuhi, hakumwona jogoo huyo. Bila shaka alimshuku mzee Kitema kwa wizi wa jogoo wake.

Alipowaambia wanakijiji wenzake juu ya kupotea kwa jogoo wake, walimhimiza apige ripoti kwa chifu mara moja. Alikwenda kwa chifu na kumwambia kuwa alishuku kuwa mzee Kitema alikuwa amemwibia kuku wake. Mzee Kitema aliposikia kuwa ameripotiwa kwa chifu, alimwambia mtoto wake. "Chifu na askari wake wakija hapa, waambie kwamba nimeenda safari ya mbali sana."

Punde si punde, chifu na askari wake waliwasili ndipohapo Kitema akajificha mvunguni mwa kitanda chake. "Baba yako yuko wapi ?" Chifu alimwuliza mtoto wa Kitema. "Baba yangu alikwenda safari ya mbali sana". Mtoto akajibu. "Baba yako atarudi lini?"; Chifu aliendelea kumwuliza mtoto huyo.

Kwa sababu hakumwambia mtoto wake ni lini angerudi, mtoto huyo aliinama mvunguni mwa kitanda na kumwuliza baba yake kwa sauti ya juu, "Baba, chifu anauliza utarudi lini?"


Compiled & supplied by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | **ORDER ANSWERS ONLINE** at www.schoolsnetkenya.com

41. Kitema alijulikana sana kwa
A. wizi wa kuku
B. ujanja wake
C. wizi wa mifugo
D. kuwachanganisha watu

42. Ni kwa nini Kitema hakushikwa kwa haraka?
A. Alikuwa akijificha sana
B. Alikuwa mwerevu sana
C. Alikuwa mweledi sana
D. Alikuwa mjanja sana

43. Ni nini kilichowajulisha watu kuwa jogoo wa pekee hakuwa?
A. Jogoo huyo hakuwika
B. Watu hawakumwona
C. Jogoo aliwika polepole
D. Jogoo aliwika kwa Kitema

44. Tunasema mjinga kama kondoo lakini mjanja kama
A. jogoo
B. kinyonga
C. sungura
D. samaki

45. Kifungu **"apige ripoti"** ni mfano wa
A. methali
B. nahau
C. kitendawili
D. fumbo

46. Kumshuku mtu ndiko kumfanyaje?
A. Kumwona akifanya jambo
B. Kusikia kuwa mtu alifanya jambo
C. Kuambiwa kuwa mtu alifanya jambo
D. Kumdhania mtu kulifanya jambo

47. Kitema alimtuma nani akadanganye?
A. Chifu
B. Polisi
C. Wanakijiji
D. Mwana wake

48. Ni kwa nini Kitema alijificha?
A. Ili asipatikane
B. Ili ajiandae kusafiri
C. Alitaka kupumzika
D. Alitaka kumficha jogoo aliyemwiba

49. Ni nani alitarajiwa kumkamata Kitema?
A. Chifu wa kijiji chao
B. Wanakijiji kwa jumla
C. Maafisa wa polisi
D. Mwanawe na askari

50. Pendekeza kichwa bora zaidi.
A. Mtoto mwongo
B. Kitema mwizi
C. Jogoo apatikana
D. Chifu na askari